# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE

RUNGWE DISTRICT COUNCIL

# TAARIFA YA MAFANIKIO YA MIAKA 4 YA UONGOZI WA SERIKALI YA AWAMU YA TANO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE-MBEYA CHINI YA MH. DR. JOHN JOSEPH POMBE MAGUFULI, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe,
S.L.P 148,
Tukuyu
Barua pepe: ded.rungwe@rungwedc.go.tz
Simu: 025-2552225/2082
Nukushi: 025-2552586

**Novemba 2019**

**TAARIFA YA MAFANIKIO YA MIAKA 4 YA UONGOZI WA SERIKALI YA AWAMU YA TANO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWECHINI YA MH.DR. JOHN JOSEPH POMBE MAGUFULI, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## 1. UTANGULIZI

### 1.1 Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe

Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ni miongoni mwa Halmashauri 7 zinazounda Mkoa wa Mbeya ikiwa na ukubwa wa kilometa za mraba 1231.86. Kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ilikuwa na Jumla ya watu 242,809 wakiwemo wanaume 115,510 na wanawake 127,299 ikiwa na kasi ya ukuaji wa idadi ya watu wa asilimia 2.7. Kwa mwaka 2019, Halmashauri inakadiriwa kuwa na Idadi ya watu ipatayo 302,430 (Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2019).

Uchumi wa Wilaya ya Rungwe hutegemea zaidi sekta ya kilimo hususani kilimo cha ndizi, parachichi, chai, kakao, kahawa, viazi mviringo, mahindi na mbogamboga na matunda ikiwa ni pamoja na mifugo ambavyo huajiri zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wa Wilaya ya Rungwe. Shughuli nyingine hujumuisha utalii katika mlima Rungwe, daraja la Mungu, Ziwa Ngosi ambalo ni ziwa litokanalo na Volkano, maporomoko ya maji ya Kaporogwe na kivutio cha Kijungu "pothole" kinachopatikana katika mto Kiwira miongoni mwa vivutio vingine. Pia, kuna shughuli za ufugaji wa nyuki, uhifadhi wa mazingira kupitia upandaji miti, biashara hususani za mazao ya kilimo na mifugo sanjari na bidhaa za viwandani, usafirishaji, madini hasa gesi asilia sanjari na uanzishwaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa ili kukuza uchumi wa kaya, kuongeza mapato ya Halmashauri na hatimaye kuboresha maisha ya mtanzania.

Pia, Halmashauri kwa kushirikiana na Serikali Kuu na wadau wa maendeleo imekuwa na jukumu la utoaji wa huduma za jamii ikiwemo elimu, afya, maji, na miundombinu ya barabara na masoko kwa kushirikiana na wananchi ambao wamekuwa wakishiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi mbalimbali inayolenga kutoa huduma bora zenye ufanisi na tija kwa jamii.

## 2. MAFANIKIO YA WILAYA YA RUNGWE KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 4 YA SERIKALI YA AWAMU YA TANO (2015 – 2019)

Tangu Serikali ya awamu ya tano ilipoingia madarakani mwaka 2015, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imefanikiwa kufanya yafuatayo ambayo yamepelekea kuendelea kuboreka kwa maisha ya wananchi wa Rungwe na Tanzania kwa ujumla;-

## 2.1 Sekta ya Afya

Sekta ya afya ni miongoni mwa sekta muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Kwa kuzingatia hilo, Serikali ya awamu ya tano imekuwa ikielekeza rasilimali fedha na watu katika kuhakikisha kuwa huduma za afya zinatolewa kwa ufanisi na tija kupitia ujenzi na ukarabati wa Hospitali, vituo vya afya na zahanati. Kwa kipindi cha miaka 4 ya Serikali ya awamu ya tano, Halmashauri imefanikiwa kujenga na kukarabati jumla ya vituo vya afya vitatu (3) ambavyo ni kituo cha afya cha Masukulu, Ikuti na Isongole na kituo cha afya cha Mpuguso ambacho kinaendelea kujengwa. Pia, Halmashauri inaendelea na uboreshaji wa mazingira ya kutolea huduma ya afya kupitia ujenzi wa wodi ya mama na mtoto ya Hospitali ya Wilaya ya Rungwe-Makandana, ujenzi wa zahanati ya Isyonje na nyinginezo.



**Picha Na.1**: Baadhi ya majengo mapya ya Kituo cha Afya Masukulu na ukarabati- Makandana Hospital

Hii imesaidia utoaji wa huduma kwa ufanisi na hivyo kumuondolea kero mwananchi ambazo alikuwa akizipata kutokana na vituo vya kutolea huduma za afya kuwa umbali mrefu ikilinganishwa na sera ya afya inayoelekeza kuwepo kwa kituo cha afya kwa kila kata na zahanati kwa kila kijiji. Upatikanaji wa dawa na vifaa tiba umeimarika kwa asilimia 98%. Pia vifo vya mama na mtoto vimepungua kutoka wastani wa vifo vya mama wajawazito 103 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2015 hadi kufikia vifo 84 mwaka 2019 na kutoka vifo 124 kwa kila vizazi hai 1000 vya watoto chini ya umri wa miaka mitano mwaka 2015 hadi kufikia vifo 67 kwa kila vizazi hai 1000 mwaka 2019 lengo likiwa ni kutokomeza kabisa tatizo hili ifikapo mwaka 2025. Wilaya ya Rungwe imevuka lengo la Kitaifa kwa kutoa huduma za Afya karibu zaidi na Wananchi. Uwiano wa huduma za Afya kwa wananchi ni 1:5,375.

## 2.2 Sekta ya Elimu

Elimu ni nyenzo ya ukombozi katika nyanja za kijamii, kiuchumi na utawala bora. Katika kipindi cha miaka 4 ya awamu ya tano, Halmashauri imefanikiwa kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ikiwa ni pamoja na ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Ntuso, ujenzi wa mabweni katika Shule za Sekondari Bulyaga, Masoko, Ikuti, na ujenzi na

ukarabati wa maboma ya vyumba vya madarasa 33 ambapo maboma 25 ni kwa shule za msingi na maboma 8 kwa shule za sekondari.Miradi hii imetekelezwa kupitia fedha za P4R (lipa kwa matokeo) ambapo hadi kufikia mwezi Julai 2019, jumla ya maboma 30 yamekamilika na yanatumika. Katika utekelezaji wa miradi hii ya P4R, Halmashauri ilipokea jumla ya Tsh 412,500,000.00 kutoka Serikali Kuu.

Pia, serikali imefanikiwa kutoa elimu bila malipo kwa shule za msingi na sekondari. Jitihada hizi zimesaidia kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa kila mwaka kutoka wastani wa wanafunzi 7,211 mwaka 2015 hadi wanafunzi 8,180 mwaka 2019. Kiwango cha ufaulu pia kimekuwa kikiongezeka kila mwaka kutoka asilimia 58 mwaka 2015 hadi asilimia 74.4 mwaka 2018 kwa shule za msingi wakati ufaulu kwa shule za sekondari umeongezeka kutoka asilimia 84.01 mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 88.9 mwaka 2018. Pia, kupitia ujenzi wa mabweni na utoaji wa elimu kwa jamii juu ya athari za mimba za utotoni, idadi ya wanafunzi wanaopata ujauzito imepungua kutoka zaidi ya wanafunzi 05 mwaka 2015 hadi mwanafunzi 01 mwaka 2019 kwa Shule za Msingi na zaidi ya wanafunzi 44 mwaka 2015 hadi kufikia wanafunzi 40 mwaka 2019 kwa shule za sekondari na jitihada zinaendelea ili kutatua tatizo hili ikiwemo ujenzi wa mabweni.

## 2.3 Sekta ya Maji

Licha ya Wilaya ya Rungwe kuwa na vyanzo vingi sana vya maji vinavyotokana na hali nzuri ya hewa na utunzaji bioanuai za mazingira, kwa miaka mingi iliyopita, wananchi wa Wilaya ya Rungwe walikuwa wakipata adha ya upatikanaji wa maji safi na salama ambapo hadi kufikia mwaka 2015, ni asilimia 67 tu ya Wananchi waliokuwa wakipata huduma ya maji safi na salama. Hii ilitokana na baadhi ya miradi ya maji kutokamilika kwa wakati ikiwemo mradi wa maji wa Masoko Group ambao haukukamilika kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuvunjwa kwa mikataba, wakandarasi kushindwa kukamilisha miradi kwa wakati na kucheleweshwa kwa malipo.



**Picha Na.2**: Ujenzi wa miradi na utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi

Hadi kufikia mwezi septemba 2019, utekelezaji wa mradi huu ulikuwa umefikia asilimia 65 na unatoa huduma ya maji kwa wananchi kwa baadhi ya vijiji ambapo mradi huu umekamilika. Mradi huu wote utakapokamilika kabla ya kuisha kwa mwaka 2019 kupitia mamlaka ya Maji (RUWASA), utasaidia jumla ya wananchi wanaopata maji safi na salama Wilayani Rungwe kuongezeka kutoka asilimia 67.7 ya mwaka 2015 hadi asilimia 86 mwaka 2019. Mathalani, kwa mwaka wa fedha 2018/19, jumla ya Tshs.3,379,723,165.70zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maji ya Simike, Nkunga, Isyonje, Ilolo na Masoko. Miradi ya Maji Nkunga, Simike, Ilolo na Isyonje imekamilika na inatoa huduma ya maji kwa wananchi.

## 2.4 Sekta ya Kilimo na Mifugo

Kwa ujumla, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe inajitosheleza kwa chakula na ziada huuzwa katika mikoa na nchi jirani za Malawi na Zambia. Kupitia mikakati thabiti ya kukifanya kilimo na mifugo kuwa cha kibiashara badala ya kilimo na ufugaji wa kujikimu, uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo umekuwa ukiongezeka kila mwaka licha ya wakati mwingine kushuka kutegemea hali ya hewa. Hii imetokana na uwepo wa huduma za ugani karibu zaidi na wananchi kupitia msisitizo na maelekezo ya uongozi wa awamu ya tano unaowataka maafisa ugani kuwatembelea wakulima na wafugaji na kutoa ushauri wa kitaalamu badala ya kutumia muda mwingi ofisini kama ilivyozoeleka.



**Picha Na.3**: Kilimo na ufugaji kwa kufuata mbinu za kisasa na kwa kuzingatia mahitaji ya soko

Pia, kwa upande wa pembejeo za kilimo, kumekuwa na mwamko mkubwa wa matumizi ya mbolea na mbegu bora zinazoleta tija kwa mkulima licha ya pembejeo hizi kutofika kwa wakati na kwa kiasi kinachohitajika. Kwa mwaka wa fedha 2015/16 jumla ya tani 13,572.8 za mbolea za viwandani zilipokelewa nakutumika ikilinganishwa na jumla ya tani 13,791.2 kwa mwaka 2017/18. Pia matumizi ya viuatilifu yameongezeka kutoka lita 15,211.4 sawa na 41% ya mahitaji mwaka 2015/16 hadi kufikia lita 23,800.8 sawa na 60% ya mahitaji. Kwa upande wa sekta ya mifugo husani ng'ombe wa maziwa, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe inaongoza katika uzalishaji wa maziwa Mkoani Mbeya ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka wastani wa lita 60,070,000 kwa mwaka kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi kufikia lita 62,500,000 mwaka 2018.

## 2.5 Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko

Hii ni miongoni mwa sekta ambazo zimekuwa zikipewa msukumo mkubwa sana kupitia Serikali ya awamu ya tano. Hii ni kwa sababu viwanda husaidia katika kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, maji, madini na misitu ikiwa ni pamoja na kutengeneza fursa za ajira na masoko kwa wananchi. Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe haipo nyuma katika utekelezaji wa azma hii ya Serikali ya awamu ya Tano katika kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda. Katika kipindi cha miaka minne ya awamu ya tano, halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo hususani sekta binafsi imefanikiwa kujenga na kuboresha jumla ya viwanda vidogo 308, viwanda vya kati 2 na viwanda vikubwa 3.



**Picha Na.4**: Kiwanda kipya cha maji cha Tukuyu Water Spring –Majinjah Co.Ltd



**Picha Na.5**: Kiwanda cha kusindika maziwa cha ASAS-Diaries Kilichopo Wilayani Rungwe

Hii imesaidia kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa Wilayani Rungwe ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo wa ajira na mapato ya Halmashauri. Miongoni mwa viwanda hivi ni pamoja na viwanda vya kuchakata chai (WATCO), viwanda vya kuchakata parachichi (KUZA, Rungwe Avocado Company na Mohamed Enterprise). Pia, Halmashauri imeendelea kuboresha miundombinu ya masoko ikiwemo soko kuu la Tukuyu, Soko la ndizi Tandale, soko la Kiwira, Machinga na Garden na sasa inaendelea na uboreshaji wa miundombinu ya masoko ya Mpuguso na Mwambenja ili kuwa na mazingira bora ya kufanyia biashara yanayojali afya za watumiaji wa bidhaa na tija kwa wafanyabiashara.

## 2.6 Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi umekuwa ukifanyika kupitia kuwajengea uwezo wananchi kuhusu ujasiriamali, biashara na kujitegemea kwa kuwahamasisha wananchi hususani vijana, akina mama na watu wenye ulemavu kujiunga katika vikundi na kuvisajili na hatimaye kupewa mitaji ya uanzishwaji wa shughuli za kiuchumi kupitia mikopo inayotolewa na Halmashauri. Kiwango cha mikopo kimeongezeka kutoka Tsh 95,898,120.70 mwaka 2015 hadi kufikia Tsh 349,900,000/- kwa Vikundi vya Wanawake 41, vikundi vya Vijana 21 na vikundi 3 vya Watu Wenye Ulemavu mwaka 2018/19. Vikundi hivi hujishusisha na shughuli za uzalishaji mali ikiwemo shughuli za kilimo, ufugaji

na baadhi wameanzisha viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao ya kilimo na vyakula vya mifugo.

## 2.7 Miundombinu ya Barabara

Usafiri kwa njia ya barabara Wilayani ni wa kuridhisha na umekuwa ukiboreka kila mwaka isipokuwa kwa sehemu chache zenye utelezi ambapo barabara ni za udongo mtupu bila changarawe. Kwa mwaka 2015/2016, wakati Serikali ya awamu ya tano inaingia madarakani, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ilikuwa na mtandao wa barabara wenye jumla ya Kilomita 725.93. Kati ya hizo, Kilomita 2.9 ni barabara ya lami, kilomita 154.43 ni barabara za Changalawe, na kilomita 568.6 ni barabara za udongo. Kwa kipindi cha miaka 4 ya uongozi wa awamu ya tano, barabara zimeendelea kutengenezwa na kukarabatiwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa madaraja matatu uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2018/19 na matengenezo yamekuwa yakifanyika mara kwa mara.



**Picha Na.6**: Ujenzi na Uboreshaji wa miundombinu ya barabara ili kurahisisha uchukuzi – Kiwira road

Aidha kwa mwaka wa fedha 2018/19 jumla ya Tshs 800,000,000.00 zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami kilomita 1.5 ambapo mpaka Septemba 2019 jumla ya kilomita 1.114 zimetekelezwa na Wakandarasi wanaendelea na ukamilishaji. Kwa mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya Tshs.6,552,571,498.00 kimetengwa kwa ajili ya kutengeneza kilomita 12.2 za barabaraza za lami na kilomita 143.15 barabara za Changalawe.

## 2.8 Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani

Ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri umekuwa pia ukiongezeka mwaka hadi mwaka tangu Serikali ya awamu ya tano ilipoingia madarakani kunakotokana na kuzuiwa kwa mianya ya upotevu wa mapato na utumiaji wa mashine za kielektroniki ambazo zimeongeza ufanisi na tija katika ukusanyaji wa mapato licha ya changamoto zitokanazo na teknolojia hii. Uwezo wa Halmashauri kujitegemea katika bajeti zake umekuwa ukiongezeka kutoka 6.9% mwaka 2016/17 hadi kufikia 9.7% mwaka 2018/19.

## 3. CHANGAMOTO

Licha ya kuwepo kwa mafanikio mengi sana toka Serikali ya awamu ya tano ilipoingia madarakani, changamoto kadha wa kadha zimekuwa zikijitokeza katika utekelezaji wa shughuli zinazolenga kuwaletea wananchi maendeleo. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na;-

i. Baadhi ya wafanya biashara wasiokuwa waaminifu kuendelea kukwepa kulipa kodi kutokana na shughuli wanazofanya.
ii. Baadhi ya wananchi kuwa na mwamko mdogo wa kushiriki katika shughuli za maendeleo hasa zile zinazohusisha utekelezaji wa miradi kupitia rasilimali zinazopatikana katika eneo husika kwa utaratibu wa "Force Account".
iii. Utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa baadhi ya maeneo umekua ukisuasua kutokana na baadhi ya viongozi wa kisiasa kuwahamasisha wananchi kutoshiriki katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa kisingizio kuwa ni jukumu la Serikali.
iv. Ufinyu wa bajeti umekuwa ni tatizo kubwa linalopunguza ufanisi katika shughuli za kuwaletea maendeleo wananchi.

Hata hivyo, Halmashauri kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, viongozi wa Kamati za maendeleo za Kata (KAMAKA) imekuwa ikiendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua wale wote wanaokwenda kinyume na matakwa ya kisheria kwa mfano ukwepaji wa kulipa kodi halali kwa Serikali.

## 4. HITIMISHO

Hakika, Serikali ya awamu ya tano imefanikiwa katika mambo mengi sana katika nyanja za kijamii na kiuchumi hususani katika sekta za afya, elimu, maji, uanzishwaji wa viwanda, miundombinu ya barabara na masoko, uwezeshaji wananchi kiuchumi na ukusanyaji wa mapato ikiwa ni pamoja na utalii na uhifadhi wa mazingira. Jitihada hizi za Serikali zimesaidia kuendelea kuboreka kwa maisha ya wananchi.

*"Shime Serikali ya awamu ya tano kwa kuonesha njia kwa vitendo na uzalendo mkubwa. Ni jukumu sasa la kila mtanzania kuhakikisha kuwa anashiriki kikamilifu kwa namna moja ama nyingine katika kujiletea maendeleo na kulinda rasilimali za Taifa letu kwa manufaa ya kizazi hiki na vizazi vijavyo".*

Pamoja tunalijenga Taifa.

Loema I Peter
**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA**
**RUNGWE**